**HOTUBA YA MHESHIMIWA WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO MKUU WA CHAMA CHA SKAUTI TANZANIA TAREHE 10 DESEMBA, 2020 - CHUO CHA MIPANGO DODOMA**

## SALAMU

- Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,
- Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Skauti Mkuu Chama cha Skauti Tanzania,
- Bi. Grace Kado, Kamishna Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania,
- Baba Askofu Gervas John Mwasikwabhila Nyaisonga, Mdhamini wa Chama cha Skauti Tanzania,
- Mufti Abubakari Zuberi - Sheikh Mkuu Tanzania, Makamu wa Rais wa Chama cha Skauti Tanzania,
- Wajumbe wa Bodi na Kamati ya Utendaji Chama cha Skauti Tanzania,
- Makamishna wa Skauti wa Mikoa na Wilaya,
- Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania.
- Waandishi wa Habari wa vyombo mbalimbali,
- Wageni waalikwa,
- Mabibi na Mabwana.

  Nawasalimu kwa salamu maalum ya SKAUTI
  **Skauti - (kiitikio Moto!)**
  **Skauti - (kiitikio Moto!)**
  **Skauti - (kiitikio Moto!)**

## SHUKRANI NA SALAMU ZA PONGEZI

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu, Kwanza kabisa,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na ukarimu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kujumuika pamoja katika tukio hili la ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Skauti.

**Pili,** naushukuru uongozi wa Chama cha Skauti kwa kunialika kuwa mgeni rasmi na pia kwa kuamua Mkutano Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania kwa mwaka 2020 ufanyike jijini Dodoma.

**Vilevile,** nitumie fursa hii kuwakaribisha wote mliofika Dodoma kwa mara ya kwanza. Karibuni sana kwenye Jiji la Dodoma ambalo pia ni Makao Makuu ya Nchi yetu. Hii ni nafasi nzuri sana ya kuutangaza Mkoa wa Dodoma kwani wajumbe wa Mkutano Mkuu ambao wanatokea nje ya mkoa wa Dodoma watapata fursa kuona mandhari nzuri ya Dodoma na kujivunia Makao Makuu ya Nchi yetu. Aidha, wenyeji watanufaika kwa ujio wenu kwa kujiongezea kipato kupitia huduma mbalimbali watakazozitoa kwa wageni waliofika Dodoma kwenye mkutano huu.

## Kumbukizi ya Marehemu Abdulkarim Esmail Shah

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,** itakumbukwa kuwa tarehe 24 Februari 2017 ilikuwa ni mara ya mwisho kukutana na uongozi wa juu wa Chama cha Skauti Tanzania. Nilialikwa na kushiriki katika Hafla ya chakula cha jioni hafla ambayo ilikuwa imeandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kuchangisha fedha za kufanikisha maadhimisho ya miaka 100 ya uskauti Tanzania.

Katika hafla ile nilikuwa na rafiki yangu, ndugu yetu Kamishna Mkuu Marehemu Abdulkarim Esmail Shah ambaye kwa sasa ametangulia mbele za haki. Marehemu Shah atakumbukwa kwa utumishi wake uliotukuka, utayari wake na ari aliyokuwa nayo katika kuwatumikia Watanzania katika kipindi alichotumikia Chama cha Skauti 2013 - 2018. Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi. **AMINA**.

## Salamu za pongezi kwa uongozi wa Skauti

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu, kama mnavyofahamu**, maadili ya chama cha skauti na wanachama wake yanatokana na muundo wa uongozi wa chama uliopo, ninawapongeza Viongozi wote wa chama kwa kujenga na kulea maadili mema, na zaidi ya yote kwa kupambana na mmomonyoko wa maadili.

Sote tunafahamu kwamba Chama hiki kimesukwa na wazee wenye hekima na busara pamoja na vijana walio tayari katika kulinda mila na desturi zetu njema. Ninafahamu kwamba, chama hiki ni chama kikongwe na chenye mtandao wa ndani na nje ya Nchi, hivyo kwa umri wake sasa ni sawa na kisima cha kale chenye kupatikana maji mwanana yafaayo kwa wote.

Nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Bi. Grace Kado kwa kuchaguliwa kwako kushika nafasi ya Kamishna Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania. Vilevile nawapongeza Makamishna wengine wote uliowateua ili washirikiane na wewe katika kutimiza majukumu yako ya Kamishna Mkuu. **Hongereni sana!**

## Salamu kutoka kwa Viongozi Wakuu wa Nchi

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu**, kabla sijaendelea na hotuba yangu, naomba mpokee salamu za pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye pia ni Mlezi wa Skauti chama cha Skauti Tanzania

pamoja na Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais. Viongozi wetu hao, wanatoa pongezi nyingi kwa chama cha Skauti kwa mkutano mkuu. Vilevile, kwa kufanya uamuzi wa kufanyia mkutano huu hapa Dodoma. **Hongereni sana!**

## Ajenda za Mkutano Mkuu

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,** nimeoneshwa hapa ajenda za kikao chenu. Moja ya ajenda ni kupokea taarifa mbalimbali za kiutendaji za chama. Ajenda hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya chama kwani inawezesha wajumbe kujitathmini na kujua walikotoka, mwelekeo na kuweza kupanga mipango ya baadaye. Ni matumaini yangu kwamba hamtapokea taarifa hizo na kukaa nazo kimya, bali mtazijadili kwa kina na pale ambapo kuna mapungufu na changamoto mbalimbali mtajadiliana kwa pamoja kuzipatia ufumbuzi.

Naamini kila kiongozi na mjumbe aliyepo hapa atashiriki kwa ukamilifu, kwa kujituma na kutoa michango kwa faida ya nchi yetu na kwa maendeleo ya chama cha Skauti Tanzania. Ninaamini mtakuwa na majadiliano shirikishi na hamtauachia uongozi wa makao makuu tu mjadala bali wote mtachangia ili kufikia maamuzi ya pamoja ya namna bora ya kutatua changamoto za chama chenu. Katika kila chama yapo mafanikio pamoja na changamoto mbalimbali, kikao hiki kizifanyie kazi hizo changamoto na kuzigeuza kuwa fursa.

## Miradi ya kujiendeleza kiuchumi

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,** nimeambiwa kuwa mnayo rasilimali watu ya kutosha ndani ya chama cha skauti. Huo ni mtaji ambao mnaweza kuutumia kwa ukamilifu kwa maendeleo ya chama. Tumieni fursa hiyo kwa kubuni miradi ya kujiongezea kipato. Miradi ambayo itawashirikisha vijana na kuwawezesha kujiajiri ili kupunguza idadi ya vijana wasiokuwa na kazi za kuajiriwa.

**Vilevile**, zipo fursa nyingi za kuanzisha miradi kama vile ufugaji wa ng’ombe wa maziwa, kuku, samaki, sungura na miradi ya kilimo cha mboga mboga na matunda pamoja na uongezaji thamani kwa mazao yanayopatikana hapa nchini. Ni matarajio yangu kwamba kupitia ubunifu na ushirikiano na asasi mbalimbali changamoto mlizonazo zitakuwa historia katika siku za usoni.

## Mpango wa Kuwafikia Skauti walio nje ya mfumo rasmi

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu** nimefurahi kusikia kuwa mmekuwa mkiwafikia vijana walioko nje ya mfumo rasmi wa shule kupitia vikundi ya “Open Troops”. Nimefurahi pia kufahamu kuwa vikundi hivyo ni rasmi na vinajishughulisha na masuala mbalimbali ikiwemo uchangiaji wa damu, kujitolea wakati wa maafa na usaidizi wakati wa maadhimisho makubwa ya kitaifa. Nitoe wito kwa chama cha skauti kutumia fursa mbalimbali zilizoko kwenye Halmashauri ili kuviendeleza vikundi hivyo kiuchumi.

**Mheshimiwa Rais wa Skauti**, nitoe wito kwa Wakuu wa Mikoa wote kushirikiana na Chama cha Skauti katika mipango yao mbalimbali ya maendeleo katika mikoa yenu. Hii

ni pamoja kuwawezesha vijana wa skauti ambao tayari wanavyo vikundi kupata fursa miradi ya vijana inayotekelezwa ndani ya mikoa yenu.

## Umuhimu wa Uzalendo

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,** kama mnavyofahamu, uzalendo ni muhimu sana katika kujenga umoja wa kitaifa. Vijana ni zaidi ya asilimia 60 ya wananchi wa Tanzania hivyo wakipata misingi mizuri ya uzalendo tutajenga Taifa imara, lenye mshikamano, nguvu na kuendelea kudumisha amani yetu. Serikali kwa kutambua hilo, kupitia Ilani ya CCM 2020-2025, imeweka msisitizo wa kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya uzalendo wa kitaifa. Suala la uzalendo ni muhimu sana kwa mustakabali na maendeleo ya Taifa lolote.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu**, nimefurahi kuona wapo skauti wenye umri mdogo katika Mkutano huu na kwamba wanachama wa chama cha skauti huanzia umri wa miaka mitano na kuendelea. Ni dhahiri kuwa malezi na makuzi ya uzalendo kuanzia utotoni yatawezesha ujenzi wa Taifa imara lenye wananchi wenye kuipenda nchi yao, kuilinda na kuithamini. Hawa ndio viongozi bora wa baadaye ambao watailinda ipasavyo na kamwe hawatakubali kuwa vibaraka wa mataifa ya ughaibuni. Nitoe wito kwa vijana wote msikubali kurubuniwa na makundi ya watu wasio na mapenzi mema na nchi yetu ambao watataka kuwatumia kwa maslahi yao binafsi na hatimaye kuhatarisha usalama na amani ya nchi yetu. Hivyo natoa wito kwa chama cha skauti kuweka mkakati wa kuhakikisha mnawafikia vijana wa rika mbalimbali katika kutoa elimu ya uzalendo.

## Kambi za Vijana:

Napenda kuwapongeza kwa utaratibu wa makambi ya vijana kwani unatoa fursa ya kujifunza uzalendo, ujasiriamali, ukakamavu na ubunifu kwa ustawi wa Taifa letu. Nisisitize kwa vijana kuwa mafunzo mnayopewa hususan ya ukakamavu yatumike kwa tija.

Vitendo vya uvunjifu wa amani na uharibifu wa miundombinu ni ukosefu wa uzalendo na kutothamini kodi za wananchi. Vijana wakilelewa katika misingi ya uzalendo watakuwa walinzi bora wa taifa letu.

## Kiapo cha Skauti

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,** nitumie fursa hii kutoa rai kwa wanachama wote wa skauti kuheshimu kiapo cha skauti ambacho kinamtaka kila mmoja awe mtiifu kwa Mungu na kwa Taifa letu. Nisisitize kuwa kiapo chenu kidhihirishwe kwa vitendo kwa kuwa mstari wa mbele kuwasaidia watu siku zote na kufanya matendo yaliyo mema siku zote. Kila mmoja kwa nafasi yake asijiingize kwenye mambo ambayo yataharibu weledi na taswira ya chama cha Skauti.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,** sote tu mashuhuda kuwa katika maafa yaliyotokea mwaka 2017 wananchi walifukiwa na kifusi huko maeneo ya Pugu jijini Dar es salaam, nimeelezwa ya kwamba vijana wa skauti walikuwa wa kwanza kufika katika eneo la tukio na kuanza kufanya shughuli za uokoaji.

Kwa dhati ya moyo wangu, ninafurahishwa sana ninaposikia vijana wa skauti wanavyojitoa katika shughuli mbalimbali za kusaidia jamii, hususan pale wananchi wetu wanapokumbwa na majanga mbalimbali. Endeleeni na moyo huo mzuri wa kujituma, na kujitolea.

**Ushirikiano na Walezi wa Mikoa na Wilaya**

Kama mnavyofahamu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya ndio Walezi wa Skauti katika maeneo yao. Nitoe wito kwa Chama cha Skauti kufanya Kazi kwa karibu na kushirikiana na walezi wenu. Ushirikiano huo utawezesha chama cha Skauti kutatua changamoto zenu sambamba na kushiriki katika fursa mbalimbali zinazojitokeza ndani ya Mkoa.

Nirudie tena kuwapongeza sana vijana wa skauti na wanachama wote kwa kuwa mstari wa mbele katika kutimiza wajibu wao bila kujali changamoto mbalimbali zinazokabili wanachama wa Chama cha Skauti Tanzania. Nawashukuruni vijana sana na kuwatakia kila la heri katika shughuli zenu za kila siku.

**Hitaji la kumilikishwa ardhi jijini Dodoma**

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,** kupitia risala yenu nimesikia mmeomba kupatiwa ardhi kwa ajili ya kujenga Kambi Kuu ya Kimataifa ambayo itakuwa na Chuo cha Ufundi, nyumba ya kulea vijana walioathirika na madawa ya kulevya, kituo cha michezo, karakana, hoteli ya mafunzo, maeneo ya utalii na utamaduni, bustani za michezo na mashamba darasa. Nawapongeza kwa hatua hii na kwa maono haya makuu ambayo yataleta tija kwa wananchi wa Dodoma.

Nipende kuufahamisha mkutano huu kuwa Serikali iko tayari kuwaunga mkono ili mfanikishe maono yenu**.** Naelekeza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye ni Mlezi wa Skauti katika Mkoa ashirikiane na Chama cha Skauti ili kuhakikisha Chama cha Skauti kinamilikishwa eneo lililotajwa na kuanza kutekeleza mipango iliyotajwa na kuweza kujitegemea kiuchumi.

**MAAGIZO NA MAENEO YA MSISITIZO**

- Chama cha Skauti, kibuni miradi mbalimbali ya kuinua kipato sambamba na kusimamia vema vitega uchumi vilivyopo kwa maslahi ya chama.

- Wakuu wa Mikoa wote ni Walezi wa Skauti Mikoa kwa nafasi zao, wakae pamoja na skauti ili kujadili na kuona namna watakavyowezesha mchakato wa upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya makambi ya vijana.

- Vijana wa Skauti kuzingatia maadili na kuwa chachu kwa wengine kuwa na mwenendo mwema. Wakati wote skauti waepuke kutojihusisha na vitendo viovu vya uvunjifu wa amani bali wawe kielelezo cha ushupavu, uchapakazi, uadilifu, nidhamu na uzalendo. Kwa nafasi zao wawe wepesi kutoa taarifa pale ambapo wamebaini kuwepo kwa vitendo viovu.

- Nitoe maagizo kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi na Vijana) ahakikishe kwamba masuala ya skauti yanaingizwa kwenye programu zote za

mafunzo kwa vijana. Aidha, mada ya uzalendo ijumuishwe kila yanapotolewa mafunzo mbalimbali kwa vijana mfano mafunzo ya ujasiriamali, urasimishaji wa biashara na upatikanaji wa mitaji. Vilevile, kila inapopatikana fursa vijana wa skauti nao washirikishwe kwenye mafunzo mbalimbali yanayotolewa kwa vijana.

- Wizara ya TAMISEMI ichukue wajibu wa kuratibu shughuli za skauti na kusisitiza ushiriki wa vijana wengi walioko shuleni na pia kuhakikisha kuwa skauti inawekewa msitititizo kwenye utekelezaji wa mitaala kuanzia shule ya msingi ili kujenga Taifa imara. Hii ni baada ya Wizara ya Elimu kukabidhi shughuli za Elimu ya Msingi na Sekondari Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**MWISHO**

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,** kwa kumalizia, naishukuru sana Kamati ya Maandalizi ya Mkutano huu, kwa kufanikisha kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa Chama cha Skauti. Aidha, niwapongeze wadau wote waliofadhili mkutano huu kwa michango yao ya hali na mali. Na sasa natamka kwamba **Mkutano Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania wa mwaka 2020 umefunguliwa rasmi.**

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**.